

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. MDC/U. 90/164/12

Tarehe: 23/05/2022.

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Mkalama anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi ya kazi ifuatayo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIKI III NAFASI 12**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV) au Sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (cheti) "NTA Level 5" katika fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Jamii kutoka chou chochote kinachotambuliwa na Serikali

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao kwa kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhufadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.

- ix. Mwenyekiti wa Vikao vya Wataalamu katika ngazi ya Kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- xii. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata.

## **MSHAHARA**


Cheo cha Mtendaji wa Kijiji III kina Mshahara wa **TGS B1** kwa mwezi

## **MASHARTI YA UJUMLA**

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri kati ya miaka **18** hadi **45**
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye Anuani na namba za simu na majina watatu ya wadhamini wanaoaminika
- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishe barua yake ya Maombi kwa kwa mwajiri wake
- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali
- *Testimonials, Provisional Results, Statements of Results* N.k hazikubaliki
- Waombaji wote waambatanishe picha mbili za "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- Waombaji wote waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **06/06/2022** saa **09:30** Alasiri.

## **Maombi yote yatumwe kwa**

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 1007,  
**SINGIDA.**

  
Asia J. Messos  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
**MKALAMA. MKURUGENZI MTENDAJI**  
**MKALAMA SHARI YA WILAYA YA MKALAMA**